David Dunford

MJI WA KIGALI.

Jiografia ya Rwanda na Kigali

Rwanda iko karibu na katikati ya Afrika na kidogo kusini ya ikweta. Inapakana na Uganda kwa kaskazini, Tanzania kwa mashariki, Burundi kwa kusini na hakika DRC kwa magharibi. Aidha, katika mpaka wa DRC na Rwanda, baina ya nchi hizi mbili, kuna ziwa la Kivu na pia bonde la mto wa Ruzizi.

Jiji kuu la Rwanda linaitwa Kigali na linapatikana katikati ya nchi. Kigali iko karibu sana na mstari wa ikweta kwenye kimo cha mita 1400-1600 juu ya usawa wa bahari. Jiji lilijengwa kati ya milima na linazungukwa na migongo ya milima minne na mabonde yao. Eneo la biashara la Kigali liko juu ya mgongo wa mlima mmoja na mtaa wa serikali uko juu ya mwingine.

Kwa ujumla ofisi na nyumba kubwa zipo juu ya migongo ya milima pia, na watu maskini wanaishi ndani ya mabonde. Aidha, kuna milima mikubwa kuliko hiyo mingine inayozingira jiji- mlima mkubwa zaidi unaitwa Mlima Kigali na ni mita elfu moja, mia nane na hamsini kutoka kwa usawa wa bahari.



Figure 1. Ramani ya Rwanda

Historia

Kigali ilianzishwa wakati wa ukoloni wa Kijerumani mwaka elfu moja mia tisa na saba kama kituo cha mwakilishi wa Afrika ya Mashariki ya Kijerumani Richard Kandt. Wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia ilivamiwa na Wabelgiji ikawa sehemu ya eneo la kuthibiti Ruanda-Urundi chini ya utawala wa Ubelgiji.

Baada ya kugawanywa kwa Ruanda-Urundi kuwa nchi mbili za Rwanda na Burundi, Kigali ikawa mji mkuu wa Rwanda mwaka 1962.

Kuanzia mwezi wa nne, mwaka elfu moja mia tisa tisaini na nne, Kigali ilikumbwa na mauaji maarufu ya Rwanda. Karibu Watutsi na Wahutu wa kadiri milioni moja waliuawa na wanamgambo wakihutu wa interahamwe na watu wachache wa jeshi la Rwanda. Ingawa, majengo mengi ya jiji la Kigali yaliharibiwa, sasa yamekaribia kujengwa tena.

Figure 2. Mabufuu ya Vichwa Vya Watutsi ambao waliuawa katika mauaji ya 1994

Wakazi na Demografia

Kwa jumla vikundi vitatu husemwa kuwa wakazi wa Rwanda: Wahutu, Watutsi na Watwaa. Wakati wa ukoloni wa Wabelgiji, hesabu ya watu mnamo mwaka elfu moja mia tisa thelathini na moja ilionyesha wakazi wa nchi ifuatavyo: asilimia themanini na nne Wahutu, asilimia kumi na tano Watutsi na asilimia moja Watwaa. Lakini, kabla ya uhuru

vita vya wenyewe kwa wenyewe vya kwanza kati ya makabila vilianza, kwa hivyo Watutsi wengi waliuawa ama walikimbilia Ng'ambo. Mnamo mwaka elfu moja mia tisa na tisini asilimia ya Watutsi ilikadiriwa kuwa tisa ama kumi.

Halafu, baada ya mauaji ya mwaka elfu moja mia tisa tisaini na nne, kati ya asilimia sabini na tano hadi tisini ya Watutsi waliuawa. Kwa hivyo, ingawa wale ambao walikimbilia Uganda na Tanzani walirudi tena Rwanda baada ya mwisho wa vita, asilimia ya Watutsi ilipunguzwa zaidi mpaka ilikuwa karibu asilimia mbili ama tatu.

Lugha

Lugha ya kitaifa na lugha ya mama kwa Warwanda wote ni Kinyarwanda ambayo ni lugha ya kibantu. Aidha, mjini na sokoni Kiswahili kinatumika lakini si lugha asilia ya Rwanda. Lugha rasmi tangu ukoloni ni Kifaransa. Baada ya vita mwaka elfu moja mia tisa tisini na nne serikali mpya iliyoongozwa na Watutsi walioishi miaki mingi Uganda ilitumia pia Kiingereza kama lugha rasmi.

Uchumi

Karibu na mji wa Kigali watu wanachimba chuma ya stani kwa udongo kwa hivyo katika miaka ya themanini, mji ulijenga karakana ya kuyesyusha stani.

Saa hizi, biashara inaongezeka nchini Rwanda na hasa katika Kigali. Majengo mengi mapya yanachomoza kila mahali katikati ya Kigali, ukiwemo mnara wa BCDI na ofisi ya Centenary House. Aidha utalii na mashirika yasiyo ya serikali yanaauni msaada muhimu kwa uchumi wa nchi.

Usafirishaji

Viwanja Vya Ndege

Mji wa Kigali una uwanja wa ndege wa kimataifa ambao ni mahali watu wanaweza kuenda ili wachukue ndege kusafiri kwenda Nairobi, Addis Ababa, Brussels, Bujumbura na Johannesburg. Pia kuna njia ya ndege ya taifa kutoka Kigali ya kwenda Cyangugu katika kusini-magharibi ya Rwanda.

Figure 3. Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kigali

Mabasi

Mara nyingi kila siku, kuna mabasi ambayo yanaondoka Kigali kuenda mahali mbalimbali Afrika mashariki. Mabasi yalio mengi yanatoka kituo cha basi cha Nyabugogo. Kwa jumla mabasi yanachukua masaa manane kufika Kampala, masaa ishirini kufika Nairobi na masaa thelathini na sita kufika Dar es Salaam.

Aidha, mjini Kigali kuna matatu ambazo zinasafiri kila mahali pa nchi na kwa miji mikubwa.

Vivutio

Sasa mji wa Kigali una hoteli za aina ya kimataifa tatu na zilijengwa ili utalii uboreshwe na pia kuauni wasafirishaji wa biashara.

Hoteli iitwayo ‘Mille Collines’, ambayo inamaanisha ‘Milima Elfu’ katika lugha ya Kifaransa, katika mtaa wa Kiyovu ilikuwa chengo cha wakimbizi katika mauaji, kwa hivyo hoteli hii imekuwa muhimu zaidi na wametengeneza sinema ambayo inaitwa ‘Hotel Rwanda’ kuhusu ‘Mille Collines.’

Hoteli nyingine iko katika mtaa wa Kacyiru na lilikuwa linaitwa ‘Le Meridien Umumbano’ lakini baada ya mauaji, kampuni ya Novotel ililinunua kwa hivyo jina lake ni ‘The Novotel Umumbano’.

Figure 4. Hoteli itwayo 'Mille Collines'

Hatimaye mjini Kigali pana ‘The Intercontinental’. Hoteli hii ilikuwa ya Wabeljiji na ilitwa ‘Les Diplomattes’ kabla ya ‘The Intercontinental’ kuinunua na kuiboresha.

Katika Kigali, aidha kuna makumbusho, majumba ya makumbusho mengi ambayo yametabarukiwa mauaji ya Rwanda yakiwemo ‘Kigali Genocide Memorial Centre’. Aidha, kuna mikahawa mingi mjini ambayo inahudumia vyakula vya aina mbalimbali.

Mjini Kigali, eneo kuu la biashara ni karibu na ‘Hotel Mille Collines’ na pia hapo ni mahali bora zaidi pa kununua vitu vyo vyote na buldani ya serikali iko juu ya mlima wa Kacyiru ambao unapakana na mlima wa eneo la biashara.

Karibu na mji, kuna vivutio vya watalii hidaya. ‘Parc National des Volcans’ inatunza mazingira ya pekee duniani penye sokwe wa milimani katika milima ya Virunga. Wako hatarini ya kuangamizwa kutokana na uwindaji na kupanuka kwa mashamba kunakopunguza mazingira wanamoishi. Ilikuwa katika hifadhi hii ambapo

Diane Fossey alikaa kujifundisha kuhusu wanyama mpaka mwaka elfu moja mia tisa themanini na tano alipouawa na mwuaji wa wanyama.

Kati ya hizi volkeno ni ziwa la Kivu. Hapo, watalii wanaweza kukaa na wanaweza kuchukua mashua kutembelea visiwa vyote ndani ya ziwa. Aidha, watu wanaweza kufanya michezo ya maji katika ziwa la Kivu lakini vifaa ni vichache.

Kwa hivyo, ni bainifu kwamba Kigali ni mji hidaya zaidi ambao una historia adhimu- mbaya na nzuri. Ukisafiri mpaka Afrika Mashiriki, Kigali ni mahali pazuri sana pa kutembelea.